

## **TANGAZO**

### **Waheshimiwa Wabunge**

Kama jinsi Mheshimiwa Waziri Mkuu alivyotutangazia, Mkutano wa Tatu wa Bunge ambao ni Mkutano wa Bajeti utaanza tarehe 19 Aprili, 2016. Sasa napenda niwatangazie Shughuli mbalimbali tutakazozifanya kwa kipindi hiki cha mpito kama sehemu ya Maandalizi ya Mkutano huo.

Pamoja na Vikao vitakavyofanyika kuanzia tarehe 8 Februari, 2016 hadi 14 Februari, 2016 kama mlivyokwisha elezwa kwenye Kamati zenu Shughuli nyingine zitakuwa kama ifuatavyo:-

1. Tarehe 14 Machi, 2016 hadi 27 Machi, 2016- Kwa kipindi cha siku kumi na nne (14) tutakuwa na Vikao vyta Kamati za Bunge mahsus kwa ajili ya Kazi za kawaida za Kamati. Vikao hivi pia vitafanyika Jijini Dar es Salaam;
2. Tarehe 29 Machi, 2016 - Kwa mujibu wa Kanuni ya 96 ya Kanuni za Bunge Serikali itawasilisha Dondoo na Randama za Vitabu vyta Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017;
3. Tarehe 30 Machi, 2016 – Kwa mujibu wa Kanuni ya 97(1)-(2) ya Kanuni za Bunge kutakuwa na Mkutano wa Wabunge wote, ambapo Serikali itawasilisha Mapendekezo ya Mpango na kiwango cha ukomo wa Bajeti ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017;

4. Tarehe 31 Machi, 2016 hadi 6 Aprili, 2016 – Kwa mujibu wa Kanuni ya 97(4) Kwa kipindi cha Siku saba (7) Kamati ya Bajeti itafanya uchambuzi wa Mapendelekezo ya Mpango na kiwango cha ukomo wa Bajeti kwa Mwaka wa fedha 2016/2017 baada ya kuwasilishwa kwa Wabunge wote;

Aidha, katika kipindi hicho hicho kwa Mujibu wa Kanuni ya 98(1) ya Kanuni za Bunge, Kamati za Kudumu za Kisekta zitatembelea na kukagua utekelezaji wa miradi iliyotengewa fedha kwa Mwaka wa fedha 2015/2016;

5. Tarehe 7 Aprili, 2016 hadi 15 Aprili, 2016 – Kwa mujibu wa Kanuni ya 98 (2) ya Kanuni za Bunge, kwa kipindi cha siku tisa (9) Kamati za Kudumu za Kisekta zitachambua taarifa za utekelezaji wa Bajeti za Wizara zinazosimamiwa na Kamati hizo;

6. Tarehe 15 Aprili, 2016- Kwa mujibu wa Kanuni ya 98(3) ya Kanuni za Bunge kutafanyika Kikao cha pamoja kati ya Kamati ya Uongozi na Kamati ya Bajeti ili kujadili mambo muhimu yaliyojitokeza kwenye Kamati za Kisekta wakati wa kujadili utekelezaji wa Bajeti za Wizara mbalimbali;

7. Tarehe 16 na 17 Aprili, 2016 Wabunge wataelekea Dodoma tayari kwa Shughuli za Mkutano wa Tatu wa Bunge ambao utaanza tarehe 19 Aprili, 2016.

**SPIKA**

5 Februari, 2016